

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SIMU: 025 - 2502260  
Fax: 025 - 2500128



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji  
S.L.P. 599  
MBEYA.

Barua pepe: mbeyaded@yahoo.com

Kumb.Na. MDC/

06.02.2019

## **YAH: TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI YA MHANDISI II (CIVIL ENGINEER II) - NAFASI - 1 NA FUNDI SANIFU UMEME ( *Electrical Technician*) NAFASI - 1**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anayo furaha ya kutangaza nafasi za Ajira ya Mkataba kwa kazi ya Mhandisi II (*Civil Engineer*) nafasi – 1 na Fundi sanifu Ufundi Umeme ( *Electrical Technicians*) nafasi - 1 katika Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

### **1.0 MHANDISI. II (CIVIL ENGINEER II) – NAFASI – 1**

#### **1.1 SIFA ZA KAZI**

1. Cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne (IV).
2. Cheti cha Degree ya Uhandisi
3. Leseni ya uhandisi iliyosajiliwa na Bodi ya Wahandisi
4. Kila Mwombaji awe na Mdamini atakayetambulishwa na Serikali ya Kijiji/Mwajiri.

#### **1.2. KAZI ZA KUFANYA**

- a) Kusimamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya majengo ya Halmashauri
- b) Kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) kwenye majengo yanayojengwa na Halmashauri
- c) Kupitia mapendekezo ya miradi (Project Proposals) Mbalimbali ya majengo yanayowasilishwa Wizarani.
- d) Kufanya ukaguzi wa majengo mbalimbali kubaini ubora wa majengo husika.
- e) Kutoa ushauri wa kitaalam kwenye majengo mapya na yanayohitaji matengenezo

#### **1.3 MSHAHARA**

**Mshahara kwa mwezi ni Tsh. 950,000/= (Kabla ya Makato)**

### **2.0 FUNDI SANIFU UMEME (*Electrical Technician*) NAFASI – 1**

#### **2.1 SIFA ZA KAZI**

1. Cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne (IV).
3. Cheti cha Diploma ya Ufundi
4. Kila Mwombaji awe na Mdamini atakayetambulishwa na Serikali ya Kijiji/Mwajiri.

## **2.3 KAZI ZA KUFANYA**

- a) Kufanya kazi zote za fani ya Umeme kwenye majengo mbalimbali ya Halmashauri
- b) Kuandaa michoro ya Umeme kwenye majengo mapya na yanayohitaji matengenezo .
- c) Kufanya kazi za kutengeneza vifaa vya Umeme.
- d) Kufanya usanifu wa miradi midogo ya Umeme, kusimamia jinsi ya kufunga mashine mpya za Umeme zinazoweka kwenye majengo yote ya Halmashauri

## **2.4 MSHAHARA**

**Mshahara kwa mwezi ni Tsh. 525,000/=.** (Kabla ya Makato)

## **4.0 MASHARTI YA JUMLA**

- a) Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wawe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.
- b) Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe na hajawahi kupatikana na kosa la Jinai au kufungwa jela.
- c) Maombi yote yaambatishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V).
- d) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya Elimu (IV au VI), Ujuzi, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
- e) “Testimonials”, “Provisional Results” “Statement of Results” hati ya matokeo ya kidato cha Nne Havitakubalika.
- f) Waombaji waliostaafishwa /Kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba.
- g) Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- h) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 11.02.2019 saa 9.30 Alasiri.
- i) Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yatumwe masjala ya Mkurugenzi Mtendaji (W) au kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya,  
S.L.P. 599,  
Mbeya.**

Imetolewa na

**Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya**